# Azimio Linalotangaza Shule Za Umma Katika mkoa ya Jefferson Kuwa Hema na Nguzo Salama Katika Wilaya

**KWA KUWA**, mahakama kuu ya muungano wa mataifa ya Amerika imetangaza kwamba hakuna shule ya umma ya wilaya inaweza kumkataa mtoto yeyote kupata elimu ya bure bilashi ya umma kwa misingi ya hali yake ya uhamiaji, aidha ;

**KWA KUWA**,wanafunzi wanazungumza lugha 136 katika shule za umma katika mkoa ya Jefferson(JCPS), asilimia 7 ya 101,000 wanafunzi, imetambuliwa kuwa na kiwango kidogo cha ustadi katika lugha ya Kiingereza (LEP), na asilimia 6 kupokea kiingereza kama lugha ya pili (ESL), aidha;

**KWA KUWA**, idadi ya wanafunzi inayohitaji huduma za lugha ya kimombo au kiingereza inazidi kuongezeka kwa kasi zaidi katika wilaya aidha;

**KWA KUWA**, asilimia 55 ya wanafunzi ni watoto wa rangi tofauti tofauti, ikiwa ni pamoja na asilimia 37 Waamerika wenye asili ya Kiafrika, asilimia 10 kutoka Spanyola, asilimia 4 wenye asili ya Bara Asia na asilimia 4 jamii mbili au zaidi, aidha;

**KWA KUWA**, shule za umma katika mkoa ya Jefferson tunadhihirisha wajibu wetu kukaribisha na kuwaelimisha wanafunzi wote bila kujali hali, tabaka na uhamiaji, inaadhimisha mchango wao kwa jamii yetu mbalimbali kujifunza, na haitatishwa kwa kutimiza wajibu huo, aidha;

**KWA KUWA**, shule za umma katika moka ya Jefferson inahakikisha kwamba shule zetu zote ni salama na ni maeneo yanayokaribisha wanafunzi wetu wote na familia zao, aidha;

**KWA KUWA**, wanafunzi mbalimbali ambao elimu yao, usalama, ustawi wa kisaikolojia, na mahusiano ya familia ni hatari kwa sababu ya hali yao ya uhamiaji ni, na itakuwa katika siku zijazo kuwa, wanajiunga na shule za umma katika mkoa ya Jefferson, waidha;

**KWA KUWA**, shirikisho la kutekeleza sheria za shughuli za uhamiaji lina uwezo wa kuathiri mazingira ya wanafunzi wote kwa njia bora, na wana haki bila kujali hali ya uhamiaji, aidha;

**KWA KUWA**, hakuna sheria ya shirikisho au serikali inayo wajibisha shule za umma kujishughulisha na rasilimali yoyote, fedha au vinginevyo, kwa utekelezaji wa sheria ya shirikisho ya uhamiaji, aidha;

**KWA KUWA**, wafanyakazi katika idara ya elimu ni mara nyingi chanzo cha na msingi wa msaada, rasilimali, na habari ili kusaidia na kuunga mkono wanafunzi na pia kusoma kwao, ikiwemo afya zao kihisia, waidha;

**KWA KUWA**,Hatuna shaka kwamba ni kwa maslahi bora ya wanafunzi, wafanyakazi, familia zao pamoja na jamii, sisi kutumika kuhakikisha kuwa wilaya inachukua hatua madhubuti kuwahakikishia wanafunzi wote pamoja na familia zao kuwa; kuharibika kwa mazingira ya elimu ambayo inaweza kuundwa kwa uhamiaji na forodha-na- utekelezaji, matendo maovu kama haya yatapingwa vikali kivyovyote vile, kwa njia ya kisheria zilizo idhinishwa

## KWA MINTARAFU HIYO, IMEAZIMIWA:

1. Bodi/jopo la elimu katika mkoa ya Jefferson linatangaza kuwa kila shule katika mkoa ya Jefferson, kuwa hema na nguzo muhimu na salama kwa wanafunzi na familia zinazotishiwa na utekelezaji wa uhamiaji au ubaguzi, kwa kiwango kikamilifu wanaruhusiwa kisheria.

2. Isipokuwa hasusan kulazimishwa na utaratibu halali wa mahakama, wafanyakazi, makandarasi, waliojitolea kusaidia pamoja na wawakilishi wa Jopo/Bodi ya elimu katika mkoa ya Jefferson hawatatumia rasilimali za wilaya kwa lengo la kuchunguza au kusaidia katika uchunguzi au kutiwa mbaroni kwa watu ambao ukiukaji wa sheria ni,au wanaweza kuwa wakaazi wasio na stakabadhi katika muungano wa mataifa ya Amerika, au kushindwa kutoa stakabadhi zilizoruhusu kibali cha ukaazi katika muumgano wa mataifa ya Amerika.

3. Wafanyakazi, wanakandarasi, waojitolea kusaidia na wawakilishi wa shule za umma katika mkoa ya Jefferson watajizuia wakitaka kujua maelezo ya uhamiaji wa mwanafunzi, mzazi au mlezi.

4. Wafanyakazi, makandarasi, wajitoleao kusaidia, na wawakilishi wa shule katika mkoa ya Jefferson hawataruhusiwa kuulizia stakabadhi za uhamiaji za mwanafunzi yeyote, mzazi au mlezi wake.

5. Wafanyakazi, makandarasi, wajitoleao kusadia na wawakilishi wa shule ya mkoa ya Jefferson hawataruhusiwa, isipokuwa kwa kulazimishwa na utaratibu halali wa mahakama, au baadaye na kupokea kutolewa saini kutoka kwa mzazi au mlezi, kufichua kwa maafisa uhamiaji na utekelezaji wa desturi au kwa mtu yeyote mwingine au kutoa taarifa yoyote juu ya uhamiaji wa mwanafunzi au familia yake.

.

6. Wafanyikazi, makandarasi, wajitoleao na wawakilishi wa shule katika mkoa ya Jefferson, hawataruhusiwa, isipokuwa kulazimika kwa amri ya mahakama au baadae kupokea kutolewa saini kutoka kwa mzazi au mlezi, kufichua kwa maafisa wa uhamiaji na utekelezaji wa kanuni au kwa mtu yeyote mwingine au kutoa taarifa yoyote juu ya uhamiaji wa mwanafunzi au familia yake kwamba imelindwa na kipwngele cha sheria katika za elimu ya familia na faragha .

7. Hakuna uhamiaji na utekelezaj wa maafisa wa forodha au sheria nyingine ya mhudumu wa uhamiaji atapata nafasi katika shule ya mkoa ya Jefferson au utekelezaji wa sheria za uhamiaji isipokuwa:

    a) Mratibu amepewa taarifa ya nia ya kuingia, na taarifa kamilifu ili Mrakibu anaweza kuchukua hatua ya kutoa kwa ajili ya usalama wa kihisia na kimwili ya wanafunzi na wafanyakazi;
    b) Wale wanaoomba kuingia kutoa sababu na ombi kwa Mrakibu, na idhini kwa maandishi, kwa muujibu wa sheria, na;

c) Mratibu huamua baada ya kushauriana, kama inafaa, na wilaya ya ushauri wa kisheria, kwamba ombi likubaliwe.

8. shule katika mkoa ya Jefferson itaendelea kutoa ushauri nasaha madhubuti wa siri kwa wanafunzi wote, ikiwa ni pamoja na wale wanaohofia nini kinaweza kutokea kwao au familia kutokana na hali ya uhamiaji, na, bila kuuliza maelezo ya uhamiaji wa mwanafunzi yeyote, mwelekeze kila mwanafunzi mwenye hofu kama hiyo kwa mashirika kuwapatia taarifa sahihi kuhusu haki na wajibu wao chini ya sheria za uhamiaji.

9. Hakuna mwanafunzi shule katika mkoa ya Jefferson atakayenyimwa fursa sawa ya huduma yoyote, elimu au vinginevyo, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa tuzo au ufadhili wa elimu unaotolewa na taasisi, kwa misingi ya hali ya uhamiaji ya mwanafunzi.

10. shule katika mkoa ya Jefferson itachangia katika azimio hili la wanafunzi katika wilaya pamoja na wazazi na wafanyakazi wote, wanakandarasi, wajitoleao na wawakilishi katika kufanikisha mawasiliano na pia kutafsiriwa katika lugha itumiwayo na shule katika kata ya Jefferson katika kutafsiri.

11. Shule katika mkoa ya Jefferson itakuwa ikipitia upya mara kwa mara sera zake zilizopo na taratibu na kurekebisha kwa kiwango kinachohitajika kwa kuzingatia azimio hili.

KWA USHAHIDI HUU, tumeweka sahihi zetu na kupiga mhuri wa bodi ya elimu katika mkoa ya Jefferson, Kentucky, itakayo rasimiwa siku ya 7 mwezi wa Februari 2017. Azimio hili litang'oa nanga kwa kuzingatia kupitishwa kwake.

Mimi,____________________________,Naibu wa katibu wa bodi ya shule katika mkoa ya Jefferson nathibitisha kwamba hapo juu ni nakala ya kweli na sahihi ya azimio lililopitishwa katika mwezi wa Februari tarehe 7 mwaka 2017. Mkutano wa bodi ya elimu katika mkoa ya Jefferson ambayo akidi iliwasilishwa na kupiga kura.

____________________________
Chris Brady
Mwenyekiti Wa Bodi

____________________________
Donna M. Hargens, Ed. D.
Mrakibu Wa Bodi